



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**WATAHINIWA 7176 KUFANYA MTIHANI WA TAIFA WA  
KIDATO CHA NNE 2024**

Jumla ya watahiniwa **7176** waliosajiliwa katika halmashauri ya manispaa ya Ilemela wataungana na watahiniwa wenzao nchini kote kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne mwaka 2024 utakaoanza **tarehe 11 hadi 29 Novemba 2024**.

Kati ya watahiniwa hao wavulana ni **3467** na wasichana ni **3709** watafanya mtihani huo, ambapo watahiniwa **6989** ni watahiniwa wa shule wasichana wakiwa **3588** na wavulana wakiwa **3401**. Na watahiniwa wa kujitegemea wapo **187** wavulana wakiwa **66** na wasichana wakiwa **121** watafanya mtihani huo wa taifa wa kidato cha nne mwaka 2024

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina jumla ya vituo **60** vilivyosajiliwa kuendesha mtihani wa taifa wa kidato cha nne (CSEE) kwa mwaka 2024, kati yake vituo **48** ni vya watahiniwa wa shule na vituo **12** ni vya watahiniwa wa kujitegemea.

Mkurugenzi Ummu Wayayu, kwa niaba ya uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, anawaomba na kuwatakiwa kila la kheri watahiniwa wote wa mtihani wa kidato cha nne mwaka 2024 na kuwakumbusha kuzingatia na kufuata taratibu zote za mtihani ili waweze kuhitimu salama.

*Mbakile*

**Violencea S. Mbakile**  
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**  
**09 Novemba, 2024**

---

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,

Tovuti: [www.ilemelamc.go.tz](http://www.ilemelamc.go.tz)